# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 986

Jina la Chapisho: Mtaala wa Elimu ya Msingi Darasa la I -VI

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-736-4

Mtaala huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Mtaala wa Elimu ya Msingi Darasa la I -VI nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MTAALA WA ELIMU YA MSINGI
# DARASA LA I – VI

## 2023

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza 2023

ISBN 978-9987-09-736-4

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Mtaala huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Mtaala wa Elimu ya Msingi Darasa la I-VI.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kutafsiri andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Kamishna wa Elimu Tanzania, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

# Yaliyomo

Orodha ya Majedwali .......... iv
Vifupisho .......... v
Shukurani .......... vi
Dibaji .......... viii

Sehemu ya Kwanza .......... 1
Utangulizi .......... 1
1.1 Usuli .......... 1
1.2 Muundo wa Elimu ya Msingi .......... 1

Sehemu ya Pili .......... 2
Dira, Malengo na Umahiri wa Jumla .......... 2
2.1 Dira ya Elimu ya Tanzania .......... 2
2.2 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania .......... 2
2.3 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la I – II .......... 2
2.4 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III – VI .......... 3
2.5 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi .......... 3

Sehemu ya Tatu .......... 5
Maudhui ya Mtaala .......... 5
3.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Umahiri Mkuu kwa Darasa la I na la II .......... 5
3.2 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo kwa Darasa la III hadi la VI .......... 5
3.3 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi .......... 6

Sehemu ya Nne .......... 19
Ufundishaji na Ujifunzaji .......... 19
4.1 Uchopekaji wa Masuala Mtambuka .......... 19
4.2 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji .......... 19
4.3 Muda wa Ufundishaji na Ujifunzaji .......... 19
4.4 Lugha ya Kufundishia na Kujifunzia .......... 21

Sehemu ya Tano .......... 22
Upimaji na Tathmini ya Ujifunzaji na Ufundishaji .......... 22
5.1 Aina za Upimaji .......... 22
5.2 Zana na Mbinu za Upimaji .......... 24

Sehemu ya Sita .......... 25
Rasilimali za Utekelezaji wa Mtaala .......... 25
6.1 Rasilimali Watu .......... 25
6.2 Rasilimali Vitu .......... 25
6.3 Samani na Majengo .......... 25
6.4 Rasilimali Muda .......... 26
6.5 Rasilimali Fedha .......... 26
6.6 Ushiriki wa Wadau .......... 26
6.7 Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Mtaala .......... 26

Bibliografia .......... 27

# Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Maeneo ya Ujifunzaji na Umahiri Mkuu kwa Darasa la I na la II......... 5
Jedwali Na. 2: Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo Elimu ya Msingi Darasa la III hadi la VI.......................................................................................... 6
Jedwali Na. 3: Umahiri Mkuu na Mahususi kwa Darasa la I hadi la II......................... 7
Jedwali Na. 4: Somo, Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Darasa la III hadi la VI.......................................................................................... 8
Jedwali Na. 5: Mgawanyo wa Muda na Vipindi Darasa la I hadi la II kwa Wiki........ 20
Jedwali Na. 6: Mgawanyo wa Muda na Vipindi Darasa la III hadi la VI kwa Wiki.... 20

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| LAT | Lugha ya Alama ya Tanzania |
| KKK | Kusoma, Kuandika na Kuhesabu |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| WyEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| SADC | Southern Afirca Development Community |

## Shukurani

Maandalizi ya Mtaala huu yamehusisha wadau mbalimbali kutoka sekta za umma na binafsi. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha upatikanaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi Darasa I-VI. Hivyo, TET inatoa shukurani za dhati kwanza, kwa Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda (Mb.). Kamati hiyo ilikuwa na wajumbe kumi (10), wakiongozwa na Mwenyekiti wake Prof. Makenya Abraham Maboko. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi kuhakikisha kuwa Mtaala huu unaandaliwa kwa wakati na unakidhi shauku ya wadau juu ya ubora wa elimu ya msingi.

Pili, shukurani ziende kwa taasisi, wizara na wadau mbalimbali wa elimu walioshiriki kutoa maoni kuhusu uboreshaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi. Baadhi ya taasisi, wizara na wadau hao ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wajumbe wa Kamati ya Mapitio ya Sera ya Elimu, wajumbe wa Kamati ya Kufanya Mageuzi Makubwa ya Elimu Zanzibar, viongozi wa dini, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Taasisi ya Elimu Zanzibar, Bodi na Menejimenti za Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Tanzania, menejimeti na wakufunzi wa Taasisi ya Sayansi ya Karume, Chuo cha Amali Zanzibar, Baraza la Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi, Baraza la Mitihani Tanzania, Chama cha Walimu Tanzania na Baraza la Watoto na Vijana Balehe Tanzania. Vilevile, wadau wengine ni wajumbe wa kamati za shule, wanafunzi wa shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu, walimu wa shule za msingi, sekondari, wakufunzi wa vyuo vya ualimu, wahadhiri wa vyuo vikuu, waajiri, wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu, Tume ya Vyama vya Ushirika, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Akademia ya Sayansi Tanzania, Benki Kuu ya Tanzania na Shirika la Chakula na Kilimo la Kimataifa.

Tatu, TET inayashukuru mashirika ya United Nations International Children's Fund, United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization, Room to Read, Right to Play, Data Vision, Plan International, Norwegian Refugees Council, Christian Social Services Commission, Global Education Link, UWEZO, Hill Packaging Ltd., Teacher Education Support Project, Madrasa Early Childhood

Programme – Zanzibar, Morale Foundation for Education and Training na Educate, kwa kufadhili hatua mbalimbali za uandaaji wa Mtaala huu.

Nne, TET inatoa shukurani za dhati kwa wataalamu wote wa elimu ya msingi kutoka ndani na nje ya TET walioshiriki kuandaa Mtaala huu. Mwisho, ingawa si kwa umuhimu, TET inaishukuru sana Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) kwa kuwezesha kazi ya uandishi, uchapaji na usambazaji wa Mtaala huu.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

# Dibaji

Mtaala wa Elimu ya Msingi Darasa I – VI umeandaliwa kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023, maoni ya wadau yaliyokusanywa na kuchakatwa kati ya mwaka 2021 na 2022 na matokeo ya uchambuzi wa maandiko kuhusu uzoefu kutoka nchi nyingine. Mtaala huu unazingatia dira ya elimu inayolenga kumwandaa Mtanzania aliyeelimika, na mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo katika kuleta maendeleo endelevu ya kitaifa na kimataifa. Vilevile, Mtaala huu umezingatia malengo makuu ya elimu pamoja na malengo ya elimu ya msingi nchini Tanzania. Kwa kuzingatia haya, Mtaala huu umeweka viwango vya utoaji wa elimu katika ngazi ya Elimu ya Msingi kwa kubainisha ujuzi, maarifa, stadi na mwelekeo atakaoujenga mwanafunzi, umahiri wa jumla, maeneo makuu ya ujifunzaji, umahiri mkuu na mahususi, njia za ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, Mtaala umebainisha muda utakaotumika katika utekelezaji, lugha ya kujifunzia na kufundishia, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na njia zitakazotumika kupima maendeleo ya mwanafunzi kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri. Hali kadhalika, Mtaala umebainisha sifa za kitaaluma na kitaalamu za mwalimu ambaye ndiye mtekelezaji mkuu wa Mtaala katika ngazi ya shule.

Pamoja na matamko mbalimbali ya kisera na miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa, Mtaala huu umezingatia nadharia za ukuaji na ujifunzaji na Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea inayosisitiza utoaji wa elimu inayomwezesha Mtanzania kujitegemea na kumudu maisha yake ya kila siku. Hivyo, utekelezaji wake utawezesha ukuaji wa mwanafunzi kimwili, kiakili, kihisia na kijamii. Ni matarajio yangu kuwa kupitia Mtaala huu, mwalimu atamwezesha mwanafunzi kujenga umahiri uliokusudiwa. Aidha, wasimamizi wote wa utekelezaji wa Mtaala na wadau wengine wa Elimu ya Msingi nchini watahakikisha kuwa elimu inayotolewa inakidhi viwango vya ubora vinavyokubalika kitaifa, kikanda na kimataifa.



Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

**Kamishna wa Elimu**

# Sehemu ya Kwanza

## Utangulizi

### 1.1 Usuli

Nchi nyingi duniani, ikiwemo Tanzania, zinatambua kwamba elimu ni haki ya kila mtoto, na hivyo zimekuwa zikifanya jitihada mbalimbali ili kuhakikisha kuwa elimu bora inatolewa kwa haki na usawa. Jitihada hizi zinafanyika kutokana na ukweli kwamba elimu ni nyenzo muhimu katika maendeleo ya kila mtoto kitaaluma, kimaadili na katika ukuzaji wa vipaji na vipawa mbalimbali. Kutokana na azma ya Taifa ya kujenga nchi yenye uchumi shindani, Serikali imelenga kujenga jamii yenye maarifa, stadi na mwelekeo chanya itakayoweza kushiriki kikamilifu katika shughuli za kimaendeleo. Pamoja na azma hiyo, Tanzania imeridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika yaani *Southern Africa Development Community* ya mwaka 1997 kuhusu elimu na mafunzo inayozitaka nchi wanachama kuwa na elimu ya lazima kwa kipindi kisichopungua miaka tisa.

Kwa kuzingatia matamko haya, Tanzania imejizatiti kutoa elimu bora na jumuishi inayozingatia Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea iliyoasisiwa mwaka 1967 na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Aidha, Mtaala huu wa Elimu ya Msingi umejikita katika ujenzi wa umahiri wa msingi katika Stadi za Karne ya 21 ambazo ni kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, fikra tunduizi, utatuzi wa matatizo na ujuzi wa kidijiti. Hivyo basi, Mtaala huu umeandaliwa kwa lengo la kuwandaa Watanzania wenye maarifa, maadili na uzalendo, stadi na mtazamo chanya katika kuchangia maendeleo ya Taifa kwa kuzingatia mabadiliko ya sayansi na teknolojia na mahitaji ya Karne ya 21. Uandaaji wa Mtaala huu umepitia hatua mbalimbali ikiwemo kukusanya maoni ya wadau, mapitio ya nyaraka mbalimbali na uzoefu kutoka nchi mbalimbali kwa lengo la kubainisha mifano bora inayoweza kutekelezeka katika mazingira ya Tanzania.

### 1.2 Muundo wa Elimu ya Msingi

Kama inavyoelekezwa na Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 Toleo la mwaka 2023, Elimu ya Msingi inatolewa kwa muda wa miaka sita (6) katika hatua mbili. Hatua ya kwanza itatolewa kwa muda wa miaka miwili na itajumuisha Darasa la I na Darasa la II. Lengo kuu la hatua hii ni kujenga umahiri katika stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Hatua ya pili itaanzia Darasa la III hadi la VI na italenga kuimarisha stadi za KKK pamoja na stadi nyingine za maisha. Mwanafunzi ataanza Darasa la I akiwa na umri wa miaka sita (6) na kumaliza Darasa la VI akiwa na umri wa miaka 11.

# Sehemu ya Pili

## Dira, Malengo na Umahiri wa Jumla

Mtaala huu umezingatia dira, malengo na umahiri unaotakiwa kujengwa kwa kila hatua ya Elimu ya Msingi.

### 2.1 Dira ya Elimu ya Tanzania

Kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo katika kuleta maendeleo endelevu ya kitaifa na kimataifa.

### 2.2 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;
(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;
(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya Taifa na dunia kwa ujumla;
(d) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;
(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;
(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa jamii, usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

### 2.3 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la I – II

Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la I – II ni kumwezesha mwanafunzi:

(a) Kukuza stadi za Kusoma, Kuandika, na Kuhesabu (KKK), ikihusisha kutumia maandishi ya Breli, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;
(b) Kukuza uwezo wa kuwasiliana kwa njia stahiki ikiwemo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na teknolojia saidizi;

(c) Kujenga uimara wa mwili, kukuza vipaji, kushirikiana na wenzake na kuwa na mtazamo chanya kuhusu kujifunza;
(d) Kukuza urazini na ujumi, kupenda na kutunza afya na mazingira pamoja na rasilimali zilizopo;
(e) Kukuza maadili na uwezo wa kuthamini na kudumisha Tunu za Taifa na utamaduni wa jamii yake pamoja na kutambua tofauti za tamaduni mbalimbali; na
(f) Kukuza uwezo wa kuchangamana katika mazingira jumuishi.

## 2.4 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III – VI

Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III hadi la VI ni kumwezesha mwanafunzi:

(a) Kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;
(b) Kufahamu, kutumia na kuthamini lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Aidha, mwanafunzi ahamasishwe kumudu angalau lugha nyingine moja ya kigeni kulingana na hali halisi ya shule yake;
(c) Kuthamini na kudumisha utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;
(d) Kukuza maarifa, uwezo wa kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;
(e) Kukuza maadili, uadilifu, na kuheshimu tofauti za imani;
(f) Kubaini na kukuza vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa;
(g) Kukuza tabia ya kuthamini na kupenda kufanya kazi;
(h) Kutambua na kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na katika maisha ya kila siku;
(i) Kukuza maarifa, ujuzi na mwelekeo wa kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na
(j) Kukuza uwezo wa kuchangamana katika mazingira jumuishi.

## 2.5 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi

### 2.5.1 Umahiri wa jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la I na la II

Umahiri wa jumla utakaojengwa na mwanafunzi wa Darasa la I na II ni:

(a) Kutumia stadi za Kusoma, Kuandika, na Kuhesabu (KKK), ikihusisha kutumia maandishi ya Breli, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;
(b) Kuwasiliana kwa njia stahiki ikiwemo Teknolojia ya Habari na

Mawasiliano na teknolojia zingine saidizi;

(c) Kushiriki katika vitendo vya kuimarisha mwili, kukuza vipaji, kushirikiana na wenzake na kuwa na mtazamo chanya kuhusu kujifunza;

(d) Kuonesha urazini na ujumi, kupenda na kutunza afya na mazingira pamoja na rasilimali zilizopo;

(e) Kuonesha maadili, kuthamini na kudumisha tunu za Taifa na utamaduni wa jamii yake pamoja na kutambua tofauti za tamaduni mbalimbali; na

(f) Kuchangamana katika mazingira jumuishi.

### 2.5.2 Umahiri wa jumla Elimu ya Msingi Darasa la III hadi la VI

Umahiri wa jumla utakaojengwa na mwanafunzi wa Darasa la III hadi la VI ni:

(a) Kutumia stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;

(b) Kutumia na kuthamini lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Aidha, mwanafunzi ahamasishwe kumudu angalau lugha nyingine moja ya kigeni kulingana na hali halisi ya shule yake;

(c) Kuonesha, kuthamini na kuheshimu utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;

(d) Kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;

(e) Kuonesha uadilifu na kuheshimu tofauti za imani;

(f) Kutumia vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa katika miktadha mbalimbali;

(g) Kuthamini na kupenda kufanya kazi;

(h) Kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na katika maisha ya kila siku;

(i) Kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na

(j) Kuchangamana katika mazingira jumuishi.

# Sehemu ya Tatu

## Maudhui ya Mtaala

Maudhui ya Mtaala huu inahusisha umahiri, maeneo ya ujifunzaji na masomo yatakayosomwa katika Elimu ya Msingi.

### 3.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Umahiri Mkuu kwa Darasa la I na la II

Maeneo ya ujifunzaji na umahiri mkuu kwa Darasa la I na la II yamejikita katika ujenzi wa lugha, mawasiliano na stadi za hisabati, utamaduni, sanaa na michezo na afya na mazingira. Jedwali Nambari 1 linaonesha maeneo ya ujifunzaji na umahiri mkuu kwa Darasa la I na la II.

**Jedwali Na. 1:** *Maeneo ya Ujifunzaji na Umahiri Mkuu kwa Darasa la I na la II*

| Na | Maeneo ya ujifunzaji | Umahiri mkuu |
|---|---|---|
| 1. | Lugha, mawasiliano na stadi za hisabati | (a) Kusoma<br>(b) Kuandika<br>(c) Kuhesabu<br>(d) Demonstrate mastery of basic English language skills |
| 2. | Utamaduni, imani, sanaa na michezo | Kuthamini utamaduni, imani, sanaa na michezo |
| 3. | Afya na mazingira | Kutunza afya na mazingira |

### 3.2 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo kwa Darasa la III hadi la VI

Maeneo ya ujifunzaji na masomo kwa Darasa la III hadi la VI yamejikita katika kumjengea mwanafunzi umahiri wa lugha na mawasiliano, hisabati, sayansi ya jamii, sayansi na teknolojia na sanaa na michezo. Jedwali Nambari 2 linaonesha maeneo ya ujifunzaji na masomo kwa Darasa la III hadi la VI.

**Jedwali Na. 2:** *Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo Elimu ya Msingi Darasa la III hadi la VI*

| Na | Maeneo ya ujifunzaji | Masomo |
|---|---|---|
| 1. | Lugha na mawasiliano | (a) Kiswahili<br>(b) English<br>(c) Kichina<br>(d) Kiarabu<br>(e) Kifaransa |
| 2. | Hisabati | Hisabati |
| 3. | Sayansi ya jamii | (a) Historia ya Tanzania na Maadili<br>(b) Jiografia na Mazingira<br>(c) Elimu ya Dini |
| 4. | Sayansi na teknolojia | Sayansi |
| 5. | Sanaa na michezo | Sanaa na Michezo |

### 3.3 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Sehemu hii inawasilisha umahiri mkuu na umahiri mahususi kwa kila hatua ya Elimu ya Msingi.

#### 3.3.1 Darasa la I hadi la II

Umahiri mkuu na mahususi kwa Darasa la I hadi la II umeainishwa katika Jedwali Nambari 3.

**Jedwali Na. 3:** *Umahiri Mkuu na Mahususi kwa Darasa la I hadi la II.*

| Na. | Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|---|
| 1. | Kusoma | 1.1 Kutambua sauti za herufi<br>1.2 Kutambua uhusiano wa sauti na herufi<br>1.3 Kusoma kwa ufasaha<br>1.4 Kusoma na kusikiliza kwa ufahamu |
| 2. | Kuandika | 2.1 Kumudu misingi ya kuandika<br>2.2 Kumudu stadi za kuandika<br>2.3 Kutumia kanuni za kuandika |
| 3. | Demonstrate mastery of basic English language skills | 3.1 Develop listening and speaking skills in different contexts<br>3.2 Develop early literacy and numeracy skills (3Rs)<br>3.3 Communicate in different contexts |
| 4. | Kuhesabu | 4.1 Kutambua dhana ya namba<br>4.2 Kutumia matendo ya kihisabati<br>4.3 Kutumia dhana za kihisabati |
| 5. | Kuthamini utamaduni, sanaa na michezo | 5.1 Kuthamini utamaduni wake na wa watu wengine<br>5.2 Kuheshimu tofauti za kiimani<br>5.3 Kuonesha matendo ya maadili<br>5.4 Kubuni kazi za sanaa<br>5.5 Kushiriki katika michezo mbalimbali |
| 6. | Kutunza afya na mazingira | 6.1 Kutunza afya yake na jamii inayomzunguka<br>6.2 Kuchunguza vitu vilivyomo katika mazingira<br>6.3 Kujilinda na mazingira hatarishi<br>6.4 Kuwa na mtazamo chanya kuhusu mazingira |

### 3.3.2 Umahiri mkuu na mahususi kwa Darasa la III hadi la VI

Umahiri mkuu na mahususi wa kila somo kwa Darasa la III hadi la VI umeainishwa katika Jedwali Nambari 4.

**Jedwali Na. 4:** *Somo, Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Darasa la III hadi la VI*

| Na | Somo | Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|---|---|
| 1. | Kiswahili | 1.1 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1.1.1 Kutambua matamshi ya sauti mbalimbali katika silabi, maneno, sentensi na habari<br>1.1.2 Kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali<br>1.1.3 Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali |
| | | 1.2 Kuonesha uelewa wa jambo alilosikiliza au kulisoma | 1.2.1 Kuonesha stadi za kusikiliza na kuelewa<br>1.2.2 Kusoma matini kwa ufasaha na ufahamu |
| | | 1.3 Kuwasilisha hoja kwa mazungumzo na kwa maandishi kulingana na muktadha | 1.3.1 Kuwasilisha hoja kwa njia ya mazungumzo katika miktadha mbalimbali<br>1.3.2 Kuandika matini mbalimbali<br>1.3.3 Kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali<br>1.3.4 Kuonesha stadi za awali za ubunifu wa kazi mbalimbali za Kiswahili |

| Na | Somo | Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|---|---|
| 2. | English | 2.1 Demonstrate mastery of basic English language skills | 2.1.1 Develop listening and speaking skills<br>2.1.2 Develop phonemic awareness and pronunciation of English letters<br>2.1.3 Develop vocabulary by relating words with objects in the environment<br>2.1.4 Use appropriate grammar and vocabulary both orally and in writing |
| | | 2.2 Comprehend oral and written information | 2.2.1 Comprehend information presented orally<br>2.2.2 Construct meaning from simple texts<br>2.2.3 Respond appropriately in a familiar communicative context<br>2.2.4 Read appropriately a variety of simple texts |
| | | 2.3 Communicate effectively in different contexts | 2.3.1 Demonstrate knowledge of the basic features of spoken language<br>2.3.2 Produce short and basic oral messages with a logical structure and intelligible pronunciation<br>2.3.3 Produce short written messages using appropriate grammar and vocabulary<br>2.3.4 Demonstrate basic skills in creative writing |

| Na | Somo | Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|---|---|
| 3. | Kifaransa | 3.1 Maîtriser les compétences langagières de base du Français<br><br>Kumudu stadi za msingi za lugha ya Kifaransa | 3.1.1 Démontrer la conscience phonémique et la prononciation des lettres francaises<br>Kujenga ufahamu wa fonimu na matamshi ya herufi za Kifaransa<br>3.1.2 Rélier des mots aux objets dans l'environnement<br>Kuhusianisha maneno na vitu katika mazingira<br>3.1.3 Maîtriser la grammaire et le vocabulaire simples<br>Kumudu sarufi na msamiati sahili |
| | | 3.2 Comprendre des informations orales et écrites<br><br>Kuonesha uelewa wa taarifa katika mazungumzo na maandishi | 3.2.1 Écouter et comprendre des informations simples présentées oralement<br>Kusikiliza na kuelewa taarifa zinazowasilishwa kwa mdomo<br>3.2.2 Lire et comprendre des textes simples<br>Kusoma na kuelewa matini sahili<br>3.2.3 Réagir de manière appropriée à un contexte familièr de communication<br>Kuonesha mwitiko sahihi katika muktadha wa kimawasiliano unaofahamika |

| Na | Somo | Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|---|---|
| | | | 3.2.4 Lire correctement des textes simples<br>Kusoma kwa usahihi aina mbalimbali za matini sahili |
| | | 3.3 Communiquer efficacement dans des divers contextes<br><br>Kuwasiliana kwa ufanisi katika miktadha mbalimbali | 3.3.1 Démontrer une connaissance des caractéristiques de base de la langue parlée et écrite<br>Kuonesha uelewa wa sifa za msingi za lugha ya mazungumzo na maandishi<br>3.3.2 Converser dans des contextes variés en utilisant la grammaire et le vocabulaire appropriés<br>Kuzungumza katika miktadha mbalimbali kwa kutumia sarufi na msamiati mwafaka<br>3.3.3 Communiquer à l'ecrit dans des contextes variés en utilisant la grammaire et le vocabulaire appropriés<br>Kuwasiliana kwa maandishi katika miktadha mbalimbali kwa kutumia sarufi na msamiati mwafaka |
| 4. | Kichina | 4.1 掌握基本汉语技能<br>Kumudu stadi za msingi za lugha ya Kichina | 4.1.1 培养汉语声母、韵母和声调的音素意识并掌握发音<br>Kumudu ufahamu wa fonimu na matamshi ya awali, mwisho, toni na *hanzi*<br>4.1.2 能够联系单词与环境中的对象<br>Kuhusianisha maneno na vitu katika mazingira<br>4.1.3 掌握简单的语法和词汇<br>Kumudu sarufi na msamiati sahili |

| Na | Somo | Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|---|---|
| | | 4.2 在对话和写作中展示对信息的理解<br>Kuonesha uelewa wa taarifa katika mazunguzo na maandishi | 4.2.1 听懂口语表达的内容<br>Kusikiliza na kuelewa taarifa<br>4.2.2 阅读和理解简单的文本<br>Kusoma na kuelewa matini sahili<br>4.2.3 在熟悉的对话环境中做出正确回应<br>Kuonesha mwitiko sahihi katika muktadha wa kimawasiliano unaofahamika<br>4.2.4 正确阅读各种简单的文本<br>Kusoma matini sahili |
| | | 4.3 在不同的语境下进行有效交流<br>Kuwasiliana kwa ufanisi katika miktadha mbalimbali | 4.3.1 展现对口语和书面语言基本特征的理解<br>Kuonesha uelewa wa sifa za msingi za lugha ya mazungumzo na maandishi<br>4.3.2 使用适当的语法和词汇在各种环境中说话<br>Kuzungumza katika miktadha mbalimbali kwa kutumia sarufi na msamiati mwafaka<br>4.3.3 在不同的语境中，使用适当的语法和词汇进行书面交流<br>Kuwasiliana kwa maandishi kwa kutumia sarufi na msamiati mwafaka |

| Na | Somo | Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|---|---|
| 5. | Kiarabu | إظهار فهم المهارات الأساسية في اللغة العربية<br>5.1 Kumudu stadi za msingi za lugha ya Kiarabu | اكتساب المهارات الأساسية للأصوات ونطق الحروف العربية وكتابتها<br>5.1.1 Kumudu ufahamu wa fonimu na matamshi ya herufi za Kiarabu na uandishi wake<br><br>ربط الكلمات بالأشياء في البيئة<br>5.1.2 Kuhusianisha maneno na vitu katika mazingira<br><br>استخدام القواعد والمفردات المناسبة شفهيا وكتابة<br>5.1.3 Kumudu sarufi na msamiati sahili |
| | | إظهار فهم المعلومات الشفوية والمكتوبة<br>5.2 Kuonesha uelewa wa taarifa katika mazungumzo na maandishi | استماع وفهم المعلومات المقدمة شفويا<br>5.2.1 Kusikiliza na kuelewa taarifa<br><br>قراءة وفهم معنى النصوص السهلة<br>5.2.2 Kusoma na kuelewa matini sahili<br><br>إظهار الاستجابة الصحيحة في سياق تواصلي مألوف<br><br>5.2.3 Kuonesha mwitiko sahihi katika muktadha wa kimawasiliano unaofahamika |

| Na | Somo | Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|---|---|
| | | | القراءة بشكل صحيح أنواعا متنوعة من النصوص السهلة<br>5.2.4 Kusoma kwa usahihi aina mbalimbali za matini sahili |
| | | التواصل الفعال في السياقات المختلفة<br>5.3 Kuwasiliana kwa ufanisi katika miktadha mbalimbali | فهم الملامح الأساسية للغة المحادثة والنصوص المكتوبة<br>5.3.1 Kuonesha uelewa wa sifa za msingi za lugha ya mazungumzo na maandishi |
| 6. | Hisabati | 6.1 Kumudu lugha ya kihisabati katika miktadha mbalimbali | 6.1.1 Kutumia dhana ya namba kuwasiliana katika miktadha mbalimbali<br>6.1.2 Kutumia matendo ya namba katika maisha ya kila siku<br>6.1.3 Kutumia stadi za vipimo katika maisha ya kila siku<br>6.1.4 Kutumia stadi za maumbo katika maisha ya kila siku<br>6.1.5 Kutumia stadi za takwimu kuwasilisha taarifa mbalimbali |
| | | 6.2 Kufikiri kimantiki katika kutafsiri na kutatua tatizo | 6.2.1 Kutumia stadi za mpangilio kufumbua mafumbo katika maisha ya kila siku<br>6.2.2 Kutumia stadi za aljebra katika maisha ya kila siku |
| | | 6.3 Kutumia maarifa na stadi za kihisabati katika fani nyingine | 6.3.1 Kutumia stadi za uhusiano wa namba na wakati katika muktadha mbalimbali<br>6.3.2 Kutumia stadi za uhusiano wa namba na fedha katika maisha ya kila siku |

| Na | Somo | Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|---|---|
| 7. | Historia ya Tanzania na Maadili | 7.1 Kulinda historia ya Tanzania, urithi na maadili ya Taifa | 7.1.1 Kumudu dhana ya historia ya Tanzania, urithi na maadili<br>7.1.2 Kumudu maarifa ya jamii inayomzunguka<br>7.1.3 Kutumia maarifa na ujuzi wa jamii inayomzunguka kusimulia asili, urithi na maadili ya jamii husika<br>7.1.4 Kutathmini ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi |
| | | 7.2 Kumudu historia ya Tanzania na maadili kabla ya ukoloni | 7.2.1 Kuelezea mifumo mbalimbali ya utunzaji na ukuzaji wa maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni<br>7.2.2 Kuelezea maendeleo ya jamii za Kitanzania na maadili yake kabla ya ukoloni |
| | | 7.3 Kumudu Historia ya Tanzania na Maadili wakati wa ukoloni 1890- 1960 | 7.3.1 Kuelezea historia ya Tanzania na urithi wakati wa ukoloni<br>7.3.2 Kulinganisha mabadiliko na mwendelezo wa maadili kabla na wakati wa ukoloni<br>7.3.3 Kuelezea jitihada za kulinda maadili ya Kitanzania dhidi ya maadili ya kigeni yaliyoletwa wakati wa ukoloni |

| Na | Somo | Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|---|---|
| | | 7.4 Kumudu Historia ya ujenzi wa Taifa la Tanzania na maadili katika kipindi cha 1961-1966 | 7.4.1 Kumudu historia ya ujenzi wa Taifa na maadili mara baada ya uhuru<br>7.4.2 Kuelezea mchango wa tunu na alama za Taifa katika kujenga umoja wa kitaifa na uzalendo<br>7.4.3 Kutumia alama za Taifa kama utambulisho wa Tanzania |
| | | 7.5 Kutathmini Ujenzi wa Taifa na maadili wakati wa Azimio la Arusha, 1967-1985 | 7.5.1 Kuelezea misingi na maadili ya Azimio la Arusha na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea<br>7.5.2 Kuelezea mchango wa Tanzania katika mapambano dhidi ya ukoloni na ukandamizaji |
| | | 7.6 Kutathmini Historia ya Tanzania na maadili wakati wa uliberali, 1986 hadi sasa | 7.6.1 Kufafanua dhana ya uliberali kwa kuhusianisha na maadili ya Kitanzania<br>7.6.2 Kutumia maarifa na ujuzi wa historia ya Tanzania na maadili ya Taifa kufanya uamuzi sahihi katika nyakati za uliberali |
| 8. | Elimu ya Dini | Itatolewa na viongozi wa dini inayohusika kwa kuzingatia mwongozo utakaotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia | Itatolewa na viongozi wa dini inayohusika kwa kuzingatia mwongozo utakaotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |

| Na | Somo | Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|---|---|
| 9. | Sanaa na Michezo | 9.1 Kubuni kazi za sanaa | 9.1.1 Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji<br>9.1.2 Kutengeneza picha<br>9.1.3 Kufinyanga maumbo mbalimbali<br>9.1.4 Kutengeneza vitu kwa kutumia makunzi mbalimbali |
| | | 9.2 Kuimarisha afya, stadi na ushindani | 9.2.1 Kumudu stadi za kazi kupitia michezo<br>9.2.2 Kumudu mazoezi ya viungo<br>9.2.3 Kucheza michezo ya asili<br>9.2.4 Kucheza michezo mikubwa |
| | | 9.3 Kutumia kazi za sanaa na michezo kwa manufaa binafsi na ya jamii | 9.3.1 Kushiriki maonesho ya kazi za sanaa na michezo katika ngazi ya jamii na Taifa |
| 10. | Sayansi | 10.1 Kumudu nadharia za kisayansi | 10.1.1 Kuonesha uelewa wa nadharia za kisayansi<br>10.2.2 Kufanya uchunguzi sahili wa kisayansi<br>10.3.3 Kuonesha uelewa wa aina za nishati na matumizi yake |
| | | 10.2 Kumudu stadi za awali za kisayansi | 10.2.1 Kufanya majaribio sahili ya kisayansi |
| | | 10.3 Kumudu matumizi ya TEHAMA | 10.3.1 Kutumia TEHAMA katika ujifunzaji |
| | | 10.4 Kubuni programu sahili za kompyuta | 10.4.1 Kubuni programu sahili za kompyuta |

| Na | Somo | Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|---|---|
| 11. | Jiografia na Mazingira | 11.1 Kumudu stadi za awali za ramani na mfumo wa jua | 11.1.1 Kutumia ramani katika maisha ya kila siku<br>11.1.2 Kuonesha uelewa wa awali wa elimu ya mfumo wa jua |
| | | 11.2 Kumudu stadi za awali za sura ya nchi na rasilimali zilizopo | 11.2.1 Kuonesha uelewa wa awali wa sura ya nchi<br>11.2.2 Kuonesha uelewa wa rasilimali asilia kuu za Tanzania<br>11.2.3 Kuonesha uelewa wa awali wa uhusiano kati ya rasilimali asilia na maendeleo |
| | | 11.3 Kumudu stadi za awali za Jiografia ya binadamu | 11.3.1 Kuonesha uelewa wa vyanzo vya taarifa za idadi ya watu na makazi<br>11.3.2 Kuonesha uelewa wa awali wa uhusiano kati ya mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali |
| | | 11.4 Kumudu misingi ya kutunza mazingira | 11.4.1 Kuonesha uelewa wa awali wa elimu ya kutunza mazingira<br>11.4.2 Kuonesha uelewa wa awali wa dhana ya tabianchi na uhusiano wake na shughuli za kiuchumi |

# Sehemu ya Nne

## Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji utahusisha mambo mbalimbali ikiwamo uchopekaji wa masuala mtambuka, mbinu, muda na lugha ya kufundishia na kujifunzia.

### 4.1 Uchopekaji wa Masuala Mtambuka

Masuala mtambuka ni miongoni mwa mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Mtaala huu. Wanafunzi watajifunza masuala mtambuka kama vile mazingira, afya, elimu jumuishi, elimu ya jinsia, elimu ya amani, maadili, haki na wajibu wa mtoto, haki za binadamu, ulinzi na usalama, usalama barabarani, elimu ya fedha, elimu dhidi ya rushwa, ushirika na masuala ya muungano. Masuala haya yatachopekwa kwenye masomo bebezi wakati wa vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uhusiano wa suala mtambuka na somo husika.

### 4.2 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Utekelezaji wa Mtaala huu utahusisha matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazolenga kumfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji na mwalimu kuwa mwezeshaji. Mwalimu atatumia mbinu zinazomshirikisha mwanafunzi katika ujifunzaji na ufundishaji kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai na uwezo wake. Mbinu zitakazotumika ni pamoja na matumizi ya michezo na sanaa, TEHAMA na teknolojia zingine saidizi, majaribio ya kisayansi, ziara za kimasomo, majadiliano, matembezi ya galari na mbinu zingine shirikishi zinazohamasisha ujifunzaji. Mtaala unasisitiza mwalimu kuwa mbunifu na mnyumbufu katika kutumia zana halisi zinazopatikana katika mazingira yake na kutengeneza mazingira ya mwanafunzi kutumia zana hizo katika miktadha ya ujifunzaji.

### 4.3 Muda wa Ufundishaji na Ujifunzaji

Mwaka wa masomo utakuwa na siku 194 sawa na wiki 39 ambao umegawanyika katika mihula miwili inayolingana. Katika kila muhula wiki mbili zitatumika kwa ajili ya upimaji endelevu na tamati. Vipindi na muda wa ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu ya Msingi utakuwa dakika 30 kwa kila kipindi kwa Darasa la I na II, na dakika 40 kila kipindi kwa Darasa la III hadi la VI. Majedwali Nambari 5 na 6 yanafafanua mgawanyo wa vipindi kwa kila darasa kwa wiki.

**Jedwali Na. 5:** *Mgawanyo wa Muda na Vipindi Darasa la I hadi la II kwa Wiki*

| **Na.** | **Umahiri** | **Darasa la I hadi la II** | |
|---|---|---|---|
| | | **Idadi ya saa kwa wiki** | **Idadi ya vipindi** |
| 1. | Kusoma | 4 | 8 |
| 2. | Kuandika | 2 dakika 30 | 5 |
| 3. | Kuhesabu | 3 dakika 30 | 7 |
| 4. | Demonstrate mastery of basic English language skills | 3 | 6 |
| 5. | Kutunza Afya na Mazingira | 1 | 2 |
| 6. | Kuthamini Utamaduni, Sanaa na Michezo | 1 | 2 |
| **Jumla ya saa na idadi ya vipindi kwa wiki** | | **15** | **30** |

**Jedwali Na. 6:** *Mgawanyo wa Muda na Vipindi Darasa la III hadi la VI kwa Wiki*

| **Na.** | **Somo** | **Darasa la III hadi la IV** | | **Darasa la V hadi la VI** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Muda** | **Idadi ya vipindi** | **Muda** | **Idadi ya vipindi** |
| 1. | Kiswahili | Saa 3 Dakika 20 | 5 | Saa 3 Dakika 20 | 5 |
| 2. | English | Saa 4 dakika 40 | 7 | Saa 4 | 6 |
| 3. | Hisabati | Saa 4 | 6 | Saa 4 | 6 |
| 4. | Sayansi | Saa 3 Dakika 20 | 5 | Saa 3 Dakika 20 | 5 |
| 5. | Jiografia na Mazingira | Saa 2 Dakika 40 | 4 | Saa 2 Dakika 40 | 4 |
| 6. | Historia ya Tanzania na Maadili | Saa 3 Dakika 20 | 5 | Saa 3 Dakika 20 | 5 |
| 7. | Sanaa na Michezo | Saa 2 Dakika 40 | 4 | Saa 3 Dakika 20 | 5 |
| 8. | Elimu ya Dini | Dakika 40 | 1 | Dakika 40 | 1 |
| 9. | Arabic/French/ Chinese | Saa 1 Dakika 20 | 2 | Saa 1 Dakika 20 | 2 |
| 10. | Kujisomea/Maktaba | Dakika 40 | 1 | Dakika 40 | 1 |

## 4.4 Lugha ya Kufundishia na Kujifunzia

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023 inaelekeza matumizi ya lugha ya Kiswahili, Kiingereza, Lugha ya Alama Tanzania (LAT) pamoja na lugha nyingine za kigeni katika elimu na mafunzo. Sera inatamka kuwa lugha ya Kiswahili itatumika kama lugha ya kufundishia katika shule zinazotumia Kiswahili na Kiingereza kitatumika katika shule zinazotumia Kiingereza kama lugha ya kujifunzia na kufundishia. Aidha, masomo ya lugha za Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa, Kichina na Kiarabu yatafundishwa kwa lugha inayohusika.

# Sehemu ya Tano

## Upimaji na Tathmini ya Ujifunzaji na Ufundishaji

Upimaji katika elimu hufanyika kwa lengo la kubaini maendeleo ya mwanafunzi kwa kutambua kile anachokijua, anachoweza kufanya, mabadiliko ya tabia na mwelekeo na kubaini changamoto anazokumbana nazo katika kujifunza ili kuzitafutia ufumbuzi. Aidha, upimaji ukitumika vyema huamsha ari ya mwanafunzi kujifunza zaidi na kuboresha ufundishaji. Kama ilivyobainishwa katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023, Mtaala huu unalenga kuimarisha upimaji na tathmini ya maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma. Mtaala huu unasisitiza mfumo wa upimaji unaotumia vigezo vinavyotambulika vya upimaji wa maendeleo ya kila siku ya mwanafunzi. Tathmini itafanyika ili kubaini kama ujenzi wa umahiri pamoja na Stadi za Karne ya 21 ikiwemo kuwajengea wanafunzi ubunifu, fikra tunduizi na uwezo wa kutatua matatizo umefanikiwa.

### 5.1 Aina za Upimaji

#### 5.1.1 Upimaji awali

Huu ni aina ya upimaji ambao utafanyika mara tu mwanafunzi anapofika shuleni kabla ya kuanza ujifunzaji na ufundishaji kwa Darasa la I ili kupima kiwango cha uelewa na umahiri alionao. Lengo la upimaji huu ni kumwezesha mwalimu kubaini mahitaji binafsi ya mwanafunzi ili aweze kumsaidia katika ujifunzaji na ufundishaji. Mwalimu atayatumia mahitaji hayo kuandaa mipango ya kuwawezesha wanafunzi kujenga umahiri uliokusudiwa. Upimaji awali pia unaweza kutumika katika kuwapanga wanafunzi katika makundi kwa kuzingatia mahitaji yao anuai. Aidha, mwalimu anaweza kutumia matokeo ya upimaji awali kujua maendeleo ya mwanafunzi kwa kulinganisha na matokeo ya upimaji mwingine wa aina ile ile baada ya kipindi fulani cha ujifunzaji na ufundishaji. Shule zinatakiwa ziwe na utaratibu wa kuwapima wanafunzi kabla ya kuanza ujifunzaji na ufundishaji kwa Darasa la I.

#### 5.1.2 Upimaji gunduzi

Upimaji gunduzi ni sehemu ya upimaji endelevu na utamwezesha mwalimu kubaini mahitaji anuai ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki. Upimaji huu utafanyika ili kumwezesha mwalimu kupata taarifa kuhusu uwezo wa mwanafunzi katika kumudu stadi mbalimbali. Taarifa za upimaji zitatumika kutoa ushauri na afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye vikwazo mahususi katika kujifunza. Ili upimaji huu uwe fanisi, mtaalamu wa afya anaweza kuhitajika hususani kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

### 5.1.3 Upimaji wezeshi

Upimaji wezeshi ni upimaji unaofanyika wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unaendelea ili kusaidia au kuwezesha ujifunzaji fanisi kwa mwanafunzi. Upimaji huu huwa ni sehemu ya ufundishaji na ujifunzaji na hivyo lengo lake ni kuwezesha ujifunzaji kuwa fanisi. Upimaji wezeshi unaweza kufanyika kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwamo kuuliza maswali, kutoa mrejesho, mwanafunzi kubaini lengo au malengo ya ujifunzaji, mwanafunzi kujipima mwenyewe au kupimwa na wanafunzi wenzake na kutumia matokeo ya upimaji tamati kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Matumizi ya mbinu hizi yatamwezesha mwalimu kubaini uelewa na changamoto zinazowakabili wanafunzi wakati mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unaendelea na hivyo kwa pamoja kuweka mikakati ya utatuzi.

### 5.1.4 Upimaji endelevu

Upimaji endelevu utahusisha upimaji wa ndani na utafanyika na kuratibiwa shuleni sambamba na ufundishaji na ujifunzaji. Mrejesho wa upimaji huu utamwezesha mwalimu kuelewa maeneo yenye changamoto ya ufundishaji na ujifunzaji na ambayo yanahitaji kutiliwa mkazo. Mwalimu atatumia upimaji endelevu kubaini mwanafunzi mwenye matatizo ya ujifunzaji ili aweze kusaidiwa. Ili kupima kama malengo ya umahiri uliokusudiwa yamefikiwa, mwalimu atatumia mbinu na zana mbalimbali kupima maendeleo ya mwanafunzi. Upimaji utazingatia malengo ya upimaji, mahitaji ya somo, mahitaji anuai ya mwanafunzi na umahiri unaokusudiwa kujengwa katika Elimu ya Msingi. Upimaji huu pia, utamwezesha mwalimu kubaini vipaji mbalimali vya mwanafunzi kama ubunifu, uchoraji, sanaa na michezo. Upimaji endelevu utachangia asilimia 30 ya upimaji wa mwisho wa Darasa la VI.

### 5.1.5 Upimaji tamati

Upimaji tamati utafanyika mwisho wa kila muhula. Upimaji huu utahusisha upimaji wa kitaifa utakaofanyika mwishoni mwa Darasa la II, IV na la VI wenye lengo la kubaini kama mwanafunzi amefikia umahiri unaotarajiwa ili avuke ngazi au darasa moja kwenda lingine. Upimaji wa kitaifa utafanyika ili kuhakikisha uthabiti na kuaminika kwa upimaji wa ndani. Aidha, upimaji huu hautakuwa wa mchujo, bali utatumika kubaini upungufu wa ujifunzaji alionao mwanafunzi ili asaidiwe kabla hajaingia darasa linalofuata. Baraza la Mitihani la Tanzania litahusika na upimaji huu ambao utachangia asilimia 70 ya upimaji wote.

## 5.2 Zana na Mbinu za Upimaji

Mtaala huu unasisitiza upimaji unaotumia zana na mbinu zinazopima nadharia na vitendo. Zana na mbinu mbalimbali za upimaji zitatumika kupima nadharia na vitendo katika tendo zima la ujifunzaji na ufundishaji. Mbinu zitakazotumika ni pamoja na bunguabongo, uchunguzi, majaribio, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi) na kazimradi. Mbinu nyingine ni majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mtihani ya mwisho. Aidha, Mtaala unasisitiza kutumia zana za upimaji na tathmini kama vile orodhahakiki, dodoso na mkoba wa kazi. Matumizi ya mbinu na zana hizi yatatofautiana kulingana na sababu ya upimaji, aina na mahitaji ya somo, mahitaji anuai ya mwanafunzi na umahiri unaokusudiwa kujengwa.

# Sehemu ya Sita

## Rasilimali za Utekelezaji wa Mtaala

Rasilimali za utekelezaji wa Mtaala huu zinahusisha rasilimali watu, vitu, samani na majengo, muda na fedha. Viwango na sifa stahiki za rasilimali hizi zinatolewa na wizara yenye dhamana kupitia miongozo mbalimbali.

### 6.1 Rasilimali Watu

Rasilimali watu inayohitajika katika utekelezaji wa Mtaala huu inajumuisha walimu mahiri na watumishi wasio walimu au wafanyakazi mwega. Aidha, mwalimu atakayefundisha Elimu ya Msingi anatakiwa awe angalau na Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi kutoka chuo kinachotambulika na Serikali. Mwalimu anatakiwa aweze kufundisha, kupima na kufanya tathmini. Sifa zaidi za mwalimu zimefafanuliwa kwenye Kiunzi cha Umahiri wa Mwalimu kilichoandaliwa na Wizara yenye dhamana ya kusimamia elimu.

Watumishi mwega ni kiungo muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa Mtaala huu. Kundi hili linajumuisha wataalamu kama vile wakutubi, wataalamu wa maabara, waganga na wauguzi, makatibu muhtasi na wasaidizi wa ofisi. Wafanyakazi hawa watapaswa kuwa wamepata mafunzo katika chuo kinachotambulika na Serikali na wamefuzu katika fani inayohusika.

### 6.2 Rasilimali Vitu

Rasilimali vitu inahusisha vifaa mbalimbali vitakavyosaidia utekelezaji wa Mtaala huu. Rasilimali hizo ni pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia ambavyo vinajumuisha mihtasari, miongozo, vitabu vya kiada na ziada na zana za kufundishia na kujifunzia. Vifaa vingine ni vifaa vya sayansi na TEHAMA kama vile vifani, vinasa sauti na kompyuta. Vilevile, rasilimali vitu inajumuisha viwanja vya michezo, vifaa vya michezo, sanaa na fani mbalimbali. Aidha, vifaa vingine muhimu kwa utekelezaji wa Mtaala huu ni vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Vifaa hivvo ni vile vya kusaidia kuona, kusikia na kugusa kama vile mashine za Breli, vitabu vya sauti, vikuza sauti na vikuza maandishi kwa wenye uoni hafifu. Ili kuthibiti ubora, vifaa vitakavyotumika shuleni ni vile vilivyothibitishwa na Wizara inayohusika na elimu.

### 6.3 Samani na Majengo

Samani na majengo ni miongoni mwa rasilimali muhimu katika utekelezaji wa Mtaala huu. Majengo yanajumuisha madarasa, maabara, karakana, maktaba,

ofisi za walimu, mabweni, kumbi, jengo la kutolea huduma za afya na jiko. Samani na majengo hayo yazingatie wanafunzi wa aina zote wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Hivyo, samani na majengo yatazingatia mwongozo uliowekwa na Wizara inayohusika na elimu.

**6.4 Rasilimali Muda**

Muda wa utekelezaji wa Mtaala huu ni miaka sita (6) yenye mihula miwili kwa kila mwaka wa masomo. Siku za masomo kwa mwaka ni 194 ambazo ni sawa na wiki 39 kama ilivyofafanuliwa katika Jedwali Nambari 5 na 6. Aidha, kalenda ya masomo itatolewa na Wizara yenye dhamana ya kusimamia elimu. Hivyo, walimu, wazazi, walezi, jamii, Serikali na wadau mbalimbali wa elimu wanatakiwa kuhakikisha kuwa muda uliopangwa unatumika vema katika kutekeleza Mtaala huu.

**6.5 Rasilimali Fedha**

Utekelezaji wa Mtaala huu utategemea uwepo wa rasilimali fedha za kutosha. Rasilimali hii itapatikana kupitia kwa wadau mbalimbali. Serikali itashirikiana na sekta binafsi pamoja na wabia wa maendeleo ya elimu katika kuhahakisha upatikanaji wa rasimali fedha ya kutosha ili kufanikisha utekelezaji wa Mtaala huu.

**6.6 Ushiriki wa Wadau**

Ushirikishwaji wa wazazi au walezi na wadau wengine wa elimu ni muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa Mtaala huu. Shule za msingi zitashirikiana na wadau hawa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa katika utoaji wa elimu ya msingi.

**6.7 Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Mtaala**

Usimamizi wa utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi ni mchakato muhimu wa kuhakikisha kuwa malengo yake yametekelezwa kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa. Mtaala huu utasimamiwa na Wizara inayohusika na elimu. Usimamizi wa Mtaala wa Elimu ya Msingi utafanywa na walimu wakuu wa shule kwa kushirikiana na kamati ya shule, maafisa elimu mkoa, wilaya, kata na wathibiti ubora wa shule wa kanda, wilaya na kata. Aidha, ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mtaala huu unalenga kupata mrejesho wa namna mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unavyofanyika ikihusisha mafanikio, changamoto na namna ya kuzitatua kwa wakati ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

# Bibliografia


Charter, A. (1990). *African charter on the rights and welfare of the child*. AU.

Halinen, I., & Järvinen, R. (2008). Towards inclusive education: the case of Finland. *Prospects*, 38(1), 77-97.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1982). Mfumo wa elimu Tanzania 1981-2000. Ripoti na maendeleo ya tume ya Rais ya Elimu: Juzuu ya Pili.

KICD. (2017). Basic education curriculum framework. Kenya Institute of Curriculum Development.

Kopweh, P. S. (2014). Curriculum development in Tanzania: an investigation of the formulation, management and implementation of the 2005 curriculum reform in selected disadvantaged districts (Doctoral dissertation, University of Glasgow).

Lakkala, S., Uusiautti, S., & Määttä, K. (2016). How to make the neighbourhood school a school for all? Finnish teachers' perceptions of educational reform aiming towards inclusion. *Journal of Research in Special Educational Needs*, 16(1), 46-56.

Mauritius Institute of Education (2015). *National curriculum framework nine year continuous*. Mauritius Institute of Education.

Ministry of Education and Vocational Training (2014). *Education and training policy*. Ministry of Education and Vocational Training.

Ministry of Education, Science and Technology (2019). *National curriculum framework for basic and teacher education.* Tanzania Institute of Education.

Ministry of Education, Science and Technology. (2022). National strategy for inclusive education in Tanzania 2021/22 -2025/26. Ministry of Education Science and Technology.

Ministry of Education and Vocational Training, (2009). National strategy on inclusive education 2009 – 2017. Ministry of Education Science and Technology.

Ministry of Education and Vocational Training. (2014). *Education and training policy (2023 Ed.)*. Ministry of Education, Science and Technology.

National Institute for Educational Development. (2016). *National curriculum for basic education*. Ministry of Education, Arts and Culture.

Nyerere J. K. (1967). *Education for self-reliance*. Government printer.

Persekutuan, P. P. K. (2013). Malaysia education blueprint 2013-2025 (Preschool to Post-Secondary Education). Kementerian Pendidikan Malaysia.

Tanzania Institute of Education. (2007). *Curriculum for ordinary level Secondary education in Tanzania*. Tanzania Institute of Education.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2022). *Ripoti ya maoni ya wadau kuhusu uboreshaji wa mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu*. Taasisi ya ElimuTanzania.

UNESCO. (1990). Joemtien World Conference on EFA. UNESCO.

The United Republic of Tanzania. (1999). The Tanzania development vision 2025. United Republic of Tanzania.

Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia. (2019). *Mtaala wa elimu ya msingi darasa la I–VII*. Taasisi ya Elimu Tanzania.